IOWA READING RESEARCH CENTER

Student Reading Success Through Research and Collaboration

# Kujifunza Kiingereza na Watoto wako na Vijana: Kutumia Barua Taka Kujizoeza Kiingereza



Na Nicole DeSalle, Mratibu wa Maandiko, Kituo cha Utafiti wa Kusoma Iowa

*Maelezo ya Mhariri: Kujifunza pamoja kunaweza kuboresha ustadi wa watoto wako na vijana wa lugha ya Kiingereza na pia yako mwenyewe. Chapisho hili ni sehemu ya safu inayoendelea iliyobuniwa kusaidia walezi ambao ni wanafunzi wa Kiingereza kupata fursa za kujifunza Kiingereza kwa familia katika maisha yao ya kila siku*

Tunaishi katika ulimwengu wa kidijitali. Na bado, katika enzi hii ya ujumbe wa maandishi na program za simu janja, sanduku lako la barua bado linaweza kujazwa mara kwa mara na barua taka kama karatasi za kuponi na matangazo. Ingawa silika yako inaweza kuwa kuweka karatasi moja kwa moja kwenye pipa la kuchakata, kuna njia za kutumia barua hiyo taka au vitu vingine vya kila siku (kwa pamoja hujulikana kama realia) kusaidia maendeleo yako ya kusoma na kuandika Kiingereza na ile ya watoto na vijana wako. Lugha inatuwezesha kutatua shida na kushirikiana na wengine kijamii (Vygotsky, 1978). Kwahivyo, kufanya mazoezi na realia kama vile kuponi na matangazo inaweza kukuruhusu wewe na watoto wako au vijana kufanya mazoezi na maingiliano yanayotokea katika maisha ya kila siku. Aina hii ya uhalisia pia inaweza kukusaidia wewe na watoto wako au vijana kupata maarifa ya kitamaduni juu ya Marekani, kama aina ya bidhaa ambazo zinaweza kupatikana kwenye maduka na aina ya habari ambayo hupatikana katika matangazo (Xu, 1999).

## Kujenga Pamoja Ufahamu wa Maelezo ya Awali

Kwa wanafunzi wa Kiingereza, maneno haya ni muhimu kujua kabla ya kujaribu shughuli kwenye chapisho hili.

- Kuna barua unayopokea ambayo unataka kupokea, kama vile barua, au kitu unachohitaji kupokea kama bili. Barua ambayo hutaki kupokea mara nyingi huitwa *barua taka*. Kuponi na matangazo ni aina ya barua taka. Ingawa matangazo na kuponi zinaweza kuwa na faida, watu wengi huzitaja kama barua taka kwasababu hupokea nyingi na kwasababu hawakuziomba. Neno taka mara nyingi hutumiwa kuelezea aina hii ya maudhui yasiyohitajika ambayo hutumwa kwa baruapepe yako. Kwa habari zaidi juu ya mada hii, soma nakala hii kuhusu barua taka kutoka kwa wavuti ya wanafunzi wa Kiingereza, *Habari za hivi punde Kingereza*.
- Kuponi ni tiketi au karatasi ndogo ambayo inakupa punguzo la bidhaa au huduma. Kuponi zinaweza kupatikana kwenye gazeti au mtandaoni. Kuponi pia hutolewa kwa njia ya barua. Ukiwa na kuponi, unaweza kupata punguzo kwa kila aina ya bidhaa, kama chakula, sabuni ya kufulia, au taulo za karatasi. Kutumia kuponi, Njoo nayo dukani tiketi ya karatasi (au ichapishe kama iko mtandaoni). Mpe keshia kuponi wakati unalipa kwenye kaunta ya malipo.




- Tangazo ni ilani kuhusu bidhaa, huduma, au tukio. Matangazo mara nyingi humaanisha kutoa punguzo au kupunguzwa kwa bei. Matangazo mengine ni pamoja na kuponi.

Unaweza kujadili maswali yafuatayo na watoto wako au vijana kwa Kiingereza au kwa lugha yako ya asili:

- *Je! Tuna barua taka katika nchi yetu ya asili? Je! Ni sawa na au tofauti na barua taka huko Marekani?*
- *Je, tuna tumia kuponi? Je! Sisi huwa tunanunua nini na kuponi?*
- Je! Hivi karibuni tulipokea tangazo kwenye barua? Ilikuwa na taarifa gani ndani yake?

Unaweza kuchagua kurejea tena baadhi ya maswali haya au yote pamoja na watoto wako na vijana kadiri unapokutana na barua taka.

## Kujenga Ujuzi Pamoja: Shughuli za Kutumia Barua taka Kujizoeza Kiingereza

Shughuli hizi hapa chini ni njia chache unaweza kutumia barua taka kama kuponi an matangazo kujizoeza Kiingereza na watoto wako na vija.

## Tengeneza kamusi ya Picha

Unaweza kukusanya kuponi nyingi na matangazo. Kuunda kamusi ya picha, zipange kwa alfabeti kwenye kitabu chakavu. Unapozipanga, onyesha kuponi na matangazo na mtoto wako au kijana atambue bidhaa hiyo kwa jina lake la Kiingereza. Kisha mwambie mtoto wako au kijana akuonyeshe kuponi ili utambue ili uweze kufanya mazoezi ya msamiati, pia. Mara tu utakapounda kamusi yako ya picha, unaweza kuitumia kufanya mazoezi mengine ya lugha ya Kiingereza kama sarufi na matamshi.

## Jioee Sarufi: Nomino zinazohesabika na zisizohesabika

Pamoja na watoto wako au vijana, tambua bidhaa zilizoko kwenye kuponi ambazo zina nomino za kuhesabika na zisizohesabika. Kwa mfano, mayai yanahesabika kwasababu unaweza kuhesabu kila moja. Pia, kawaida huuzwa katika kifurushi na nambari maalum kama 12 (pia inajulikana kama dazeni). Kwa upande mwingine, nafaka haiwezi kuhesabiwa kwasababu itakuwa ngumu au haiwezekani kuhesabu kila flake au kipande cha nafaka. Na, badala ya kuuzwa kwa nambari unaweza kuhesabu kwa mkono, nafaka inauzwa kwa kiwango kilichopimwa kama boksi la onzi 12 la nafaka. Ifuatayo, tumia kuponi kutengeneza orodha ya mboga. Pamoja na mtoto wako, zunguushia duara nomino zinazohesabika: tofaa, ndizi, taulo za karatasi, n.k Chora sanduku kuzunguka nomino zisizohesabika: maziwa, mkate, sabuni

**Zoezi zaidi:** Pamoja na watoto wako au vijana, panga vitu kwenye orodha yako ya vyakula katika vikundi vilivyoandikwa, kama "mazao," "wasafishaji wa kaya," na "maziwa." Kwa mfano, maziwa na jibini ni aina ya bidhaa za maziwa. Andika neno "maziwa" kwenye orodha yako na upigilie mstari. Kisha andika "maziwa" na "jibini" chini yake. Muulize kijana wako au mtoto:

*Mazao gani mengine ya maziwa?*

## Jizoeze Matamshi: Yanayoishia na Konsonanti (s)

Pamoja na watoto wako au vijana, ainisha mazazo kwenye kuponi yanayoishia na herufi “s,” kama vile “mayai,”“keki ndogo,”“taulo za karatasi,”na “ndizi.”Herufi “s” inatumika kukufanya kitu kuwa wingi. Elezea kwamba neon linapoishia na irabu au sauti ya konsonanti kama “m, “n,”“ng,”“l,”“b,”“d,”“g,”“v,” r”,” au sauti “th,” herufi “s”inaongezwa kutengeneza wingi wa neno na ina sauti ya /z/. Sema neno “mayai,” kusisitiza sautii ya /z/ mwishoni mwa neno.

Kasha elezea kwamba neon linapoishia bila ya sauti kama “p,”“t,”“k,”“f,” au isiyo na sauti “th”, herufi “s” ina sauti ya /s/. Sema neno “keki ndogo,” sisitiza sauti /s/.

Amueni pamoja iwapo kila kuponi inayoishia na konsonanti “s” inapaswa kutamkwa na sauti /z/ au/s/.

## Jizoeze Ujuzi wa Kuzungumza: Uliza na Jibu Maswali (Kiasi Gani?)

Pamoja na watoto wako au vijana, mfanye igizo la kuwa mteja na keshia. Tumia sentensi zilizotengenezwa hapo chini kujizoeza kuuliza na kujibu maswali kuhusu kuponi kutoka kwenye kamusi yako ya picha. Kasha mbadilishane majukumu.

### Miundo ya Sentensi ili kujizoeza Kuzungumza Kiingereza

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Swali:** | Je! Ni kiasi gani naweza kuokoa kwenye _____________na kuponi hii? | **Mifano:** | *Je! Ni kiasi gani naweza kuokoa kwenye **ndizi** na kuponi hii?*<br><br>*Je! Ni kiasi gani naweza kuokoa kwenye **nafaka** na kuponi hii?* |
| **Jibu:** | Unaweza kuokoa _______. | **Mifano:** | *Unaweza kuokoa senti **39**.*<br>*Unweza kuokoa dola **12**.* |

Muafaka huu wa sentensi utakuruhusu wewe na watoto wako au kijana kufanya mazoezi ya nomino zinazohesabika na zisizohesabika (tazama Sarufi ya Mazoezi: Nomino zinazohesabika na zisizohesabiwa hapojuu). Unapofanya mazoezi, kumbuka kwamba nomino zinazohesabika zinaweza kuishia na herufi “s” wakati nomino zisizohesabika haziwezi. Kwamfano, neno "ndizi" ni nomino inayohesabika wakati neno "nafaka" ni nomino isiyohesabika. Muafaka huu wa sentensi pia utakuruhusu wewe na mtoto wako au kijana ujizoeshe kutamka konsonanti za mwisho (tazama Matamshi ya Mazoezi: Kumaliza Konsonanti (s) hapojuu). Kumbuka kwamba maneno yaliyo na konsonanti inayoishia na "-s" yanaweza kuishia na sauti ya / s / au / z /. Kwamfano, neno "senti" linaishia na / s / sauti wakati neno "dola" linaishia na sauti ya / z /.

## Jizoeze mazungumzo ya Kiingereza

Waambie watoto wako au vijana kuwa unaenda safari ya mwisho wa wiki. Amueni pamoja mtaenda wapi. Waambie:

*Tunaweza tu kuleta vitu vitatu pamoja nasi. Tunapaswa kuleta nini?*

Na watoto wako au vijana, amuaeni ni vitu vipi vitatu vilivyoonyeshwa kwenye kamusi yako ya kuponi ambavyo vitakuwa muhimu zaidi katika safari yako ya mwisho wa wiki. Kwakweli unaweza kuzingatia kiwango cha akiba kwenye kuponi kwenye uamuzi wako. Unapozungumza na watoto wako au vijana, jaribu kutumia na kutamka kwa usahihi nomino zinazohesabika na zisizohesabika.

**Kumbuka:** Kumbuka kuwa wakati unafanya mazoezi ya mazungumzo ya Kiingereza na watoto wako au vijana, ni sawa kwako kutumia maneno, misemo, au sentensi katika lugha yako ya nyumbani ikiwa haujui kusema kitu kwa Kiingereza au ikiwa neno au wazo linahitaji maelezo zaidi. Kuingiza lugha ya nyumbani inaweza kuwa njia bora ya kukamilisha kazi na kusaidia ujifunzaji wa mapya yaliyomo katika lengo au lugha mpya (Genesee &Lindholm-Leary, 2012). Lengo la mazoezi ya mazungumzo ni kupata fursa nyingi za kutumia Kiingereza kadri uwezavyo. Unaweza kujikuta ukitumia Kiingereza zaidi kila unapozungumza.

Wakati wa kujifunza lugha mpya na utamaduni mpya, vitu unavyokutananavyo katika maisha ya kila siku vinaweza kutoa fursa mpya za kujifunza. Barua taka ni njia moja ya kutumia Kiingereza bure na vifaa unavyoweza kupata ndani ya sanduku lako la barua.

Kwa mazoezi zaidi, jaribu moja ya hizi Shughuli kwaajili ya Kutumia barua Taka katika Chumba cha darasa cha ESL/EFL Classroom kutoka kwenye wavuti *The Internet TESL Journal*.

## Marejeo

Genesee, F., & Lindholm-Leary, K. (2012). The education of English language learners. In K. R. Harris, S. Graham, T. Urdan, A. G. Bus, S. Major, & H. L. Swanson (Eds.), *APA handbooks in psychology®. APA educational psychology handbook, Vol. 3. Application to learning and teaching* (pp. 499–526). American Psychological Association.https://doi.org/10.1037/13275-020

Vygotsky, L.S. (1978). *Mind in society: The development of higher psychological processes*. (M. Cole, V. John-Steiner, S. Scribner, & E. Souberman, Eds.). Harvard University Press.

Xu, Hong. (1999) Young Chinese ESL children's home literacy experiences. *Reading Horizons: A Journal of Literacy and Language Arts*, *40*, 47–64.https://scholarworks.wmich.edu/reading_horizons/vol40/iss1/3